Mashairi ya Masaibu ya Karbala

Compiled by Unknown

Al-Islam.org

Publisher(s):

Ahlul Bayt (a.s.) Assembly of Tanzania [3]

Kitabu hiki kina mashairi yaliyoandikwa juu ya janga ya karbala.
Washairi wameandika kwa ustadi sana matukio yaliyotokea Karbala ambayo huleta machozi machoni mwetu. Msomaji lazima ataguswa na mashairi haya ya kusikitisha na kuhuzunisha.

Category:

Imam al-Husayn and Karbala [4]
General [5]

Topic Tags:

Muharram [6]

Miscellaneous information:
Mashairi ya Masaibu ya Karbala Kimetolewa na Ahlul Bayt [a.s.] Assembly of Tanzania P O Box 75215 Dar es Salaam - Tanzania Kimechapwa na Bilal Muslim Mission of Tanzania S.L.P. 20033 Dar es Salaam – Tanzania

Featured Category:

Introducing the Ahlul Bayt [7]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) asema:

"Ee Allah! Hawa (Ali, Fatima, Hasan na Husain) ndio Ahlul Bait wangu, basi watoharishe kwa tohara kamili."

"Husain anatokana na mimi na mimi ninatokana na Husain..."

"Hao (Hasan na Husain) ni maua yangu katika dunia."

"Ewe Mwanangu (Husain)! Mwili wako ni mwili wangu na damu yako ni damu yangu;"

"(Ewe Husain), wewe u Sayyid, mwana wa Sayyid, na ndugu wa Sayyid; wewe u uthibitisho (wa Mwenyezi Mungu) mwana wa uthibitisho (wa Mwenyezi Mungu) na ndugu wa uthibitisho (wa Mwenyezi Mungu); na baba wa uthibitisho tisa ambao wa tisa wao ni Qaim wao ambaye atakuwa al-Mahdi."

"Hasan na Husain ni Masayyidi wa Vijana wa Peponi."

"Ewe Mola wangu! Mpende yule ampendaye Husain."

"Adhabu atakayoipewa yule muuaji wa Husain huko Motoni itakuwa sawa na nusu (nzima) ya adhabu yote watakayopewa wenye dhambi wa ulimwengu."

"...., Allah hujirafikisha na wale wajirafikishao na Husain, yu adui wa wale walio maadui zake."

"Yeyote awapendaye Hasan na Husain amenipenda, na yeyote anayewachukia amenichukia."

****

Ahlul Bayt (a.s.) Assembly ya Tanzania (ABATA), inayo furaha kwa kutoa Kitabu hiki cha Mashairi kwa watu wazungumzao Kiswahili. Yakiwemo mapendekezo ya Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi, Mwenyekiti wa ABATA, kwamba tuchapishe vitabu vya Majlis na Mashairi (Nauha na Utenzi) juu ya "Masaibu ya Karbala."

Kwa hiyo mwezi Aprili, 1998 tulichapisha Kitabu cha Majlis kinachoitwa, "Maombolezo ya Kifo cha Imam Husain (a.s.)" ambacho kimetokea kupendwa sana Afrika ya Mashariki. Alhamdulillah.

Sayyid Murtaza Rizvi na Sheikh Abdul-Majid Nassor, kwa ushauri wa Mwenyekiti wa ABATA, wameyakusanya Mashairi haya kutoka sehemu mbalimbali, wakayapanga na kupata kitabu kiitwacho "Mashairi ya Masaibu ya Karbala" ambacho unacho mkononi mwako hivi sasa.

Hiki ni Kitabu cha tatu ambacho kimetolewa na Ahlul-Bayt (a.s.) Assembly ya Tanzania, na tunayo furaha kubwa kutoa kitabu cha Mashairi ya Karbala kwa Kiswahili ambacho ni cha kwanza katika lugha ya Kiswahili.

Allah Subhanahu wa Ta'ala atoe malipo yake kwa wale wote ambao wamesaidia katika uchapishaji wa kitabu hiki.

Wamaa Tawfeeqi Illa Billah.
P.O. Box 75215
Dar es Salaam
Tanzania
24, Februari, 1999

F. A. Hameer
Katibu Mkuu
Ahlul-Bayt (a.s.) Assembly ya Tanzania

Limetungwa na:
Maallim Abdul Qahari bin Said,

(wa Mtama, Lindi – Tanzania)

Utangulizi

Marehemu Maallim Abdul Qahari bin Saidi mwanachuoni mashuhuri wa Madhehebu ya Sunni (Shafii) ndiye aliyeandika shairi hili.

Kwa sauti kubwa na shangwe alilisoma shairi hili katika adhimisho la Siku ya Imamu Husain (a.s.) lililofanyika huko Mtama (Lindi, Tanzania) mnamo tarehe mosi Julai mwaka 1961.

Lilirekodiwa katika "Tape Recorder" na kusikilizwa katika miji mingi mingineyo barani Afrika.

Vile vile liliwahi kuchapishwa mara mbili na "Imamia Mission" ya Lucknow, India.

Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain

Bismillah nitajayo, Ni jina la Mola wangu,
Rahmani isemwavyo, Ya akhera na ulimwengu,
Rahimi isimuliwavyo, Akhera ya wacha Mungu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Alhamdu ni sifa za Mola, Lillahi jina la Hadhiya,
Namwalia Rasula, Salaam na neema pia,
Waalaalihi liula, Zienee kwa wote pia,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Baada ya kumaliza, Sasa natunga shairi,
Naanza kujituliza, Nitaje kisa na maamuri,
Kidogo nitatambaza, Si sababu ya kujitafakhari,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ilahi kamtuma Rasuli, Muhammadi Liamini,
Awe mtetezi kamili, Aidhihirishe dini,
Nae kakubali, Kuwa kiongozi wa dini,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Kisa ninachoeleza, Maendeleo yaamini,
Agizo alitimiza, Alimtuma Manani,
Hakuna la kumtatiza, Mwislamu moyoni,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wakati wa maisha yake, Muhammadi Rasuli,
Alimzaa mtoto mke, Fatimati Libatuli,
Kamuoza binami yake, Imamu Sayyidna Ali,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mola mjuwa falagha, Ali akamzaa Husain,
Mwenyezi Mungu Kawapanga, Wajukuu zake amini,
Dunia ikawa na mwanga, Wakafurahi Malaika mbinguni,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Siku nyingi zikapita, Mustafa akatawafu,
Ndipo kuanza matata, Shamu mambo machafu,
Nakuzitangaza vita, Kuazimu ushupavu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Dini ikavurugwa, Kwa vitendo vya Yazidi,
Amani zikapotea, Maasi yakazidi,
Kidogo wafuatao njia, Ya Nabii Muhammadi,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikawa nyakati hizo, Zikapunguka imani,
Ikakithiri michezo, ya hali ya kishaitwani,
Wachache wafuatao nguzo, Nakuthibiti imani,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Na hali hapo zamani, Nabii alitamka,
Ya Husain minni, Wa–ana ilaika,
Ndipo kasimama Husain, Na amri akazishika,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Haki ikasimama, Na batili zikaondoka,
Mpaka siku ya Kiyama, Dini zitabadilika,
Fahimma hata Fahhama, Uislamu utatajika,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Na kifo chake kwa kamili, Ni fidia ya Uislamu,
Mfano wa Ismaili, Kwa Nabii Ibrahima,
Dini leo ni kamili, Imesimama salama,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Imamu aliposikia, Ilivyobadilika Shamu,
Aamuruvyo bini Muawiya, Mambo mengi ya haramu,

Na dini imepotea, Anadai na Uimamu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Imamu moyo ukasita, Akifikiri tarafa,
Yazidu anazozipita, Bila ya amali nadhifu,
Akasema haihata, Ila nende zangu Kufa,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Tarekhe ishirini na Nane, Akaondoka Madina,
Kwenda kulitufu Kaaba, Sharia iliyo bayana,
Yazidi Kakutubu kitaba, Kujisainisha laana,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Barua ya kutoka Shamu, Ikafika mjini Makka,
Kaarifiwa hakimu, Husain muuwe haraka,
Husain alipofahamu, Ikambidi kuondoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Imamu Husain ashirafu, Baada hayo kufahamu,
Akasema Makka ni tukufu, Kutia damu haramu,
Hicho ni kitendo dhaifu, Kakataza Rabi Karimu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikawa tarehe pili, Ya mwezi wa mfunguo nane,
Karbala akawasili, Kiasi cha saa nane,
Majeshi ya wakatili, Yakazuia maji wasinywe,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mpaka tarehe saba, Mtoni kuna hatari,
Maadui wameziba, Na maneno ya jeuri,
Maji heri kunywa simba, Nguruwe na makafiri,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Islamu Kataharaki, Kooni kulikauka,
Kila akiwalahiki, Maji yao kuwataka,
Wao kuzidi hamaki, Huruma imewatoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mama mtoto taabani, Maziwa yamekauka,
Hamna tone kifuani, Mtoto anahangaika,
Kayabisika midomoni, Damu zinamdondoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wamezuia hayo maji, Watu elfu tano,
Wengi mno walindaji, Wa mishale bila mifano,
Ingawa anawahitaji, Wala hawana mapatano,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikipika siku tatu, Tangu waponyimwa maji,
Wameshikana hao watu, Kwa hali ya uziwiyaji,
Wakaona hiyana si kitu, Wana nia ya uuwaji,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Tarehe tisa ilipofika, Walitaka waanze vita,
Imamu Husain aliwataka, Ruhusa ya swala kupata,
Amuabudu Rabuka, Bila kumfika matata,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mkuu wa jeshi la Yazidi, Ana moyo mughaladha,
Omar bini Saadi, Ameajiriwa kwa fedha,
Akishatimiza ahadi, Hataki kwa Mungu Karadha,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Asubuhi tarehe kumi, Vita ikaumuka,
Ndipo kuanza uvumi, Mishale kuipachika,
Omari mtaka dami, Mshale ukamtoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ndiye mwamrishaji, Vita kuamrisha,
Hakuna tena mkaaji, Muda wao umekwisha,
Hakuna tena kuhoji hoji, Kawamalizeni maisha,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikawa hekaheka, Hali ya vita ni kali,
Islamu kateseka, Maji yamewawiya mbali,
Mradi wana mashaka, Hawanywi wala hawali,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Alipofika mkatili, Mlaanifu mwingi wa balaa,
Na kisu chake kikali, Yuna kwitwa Shimr,
Imam aliomba aswali, Hakupenda amalize swala,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Alipotaka amuuwe, Alitamka Imamu,
Ebu nikuchungue, Nikujue mjirimu,

Akaona uso wa Nguruwe, Mara alimfahamu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Aliambiwa zamani, Uhai wa babu yake,
Atayemuua Husain, Atabadilika sura yake,
Awe mnyama wa mwituni, Nguruwe kwa jina lake,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikaja nyingi tufani, Ikatokea kusini,
Jua likazama mbinguni, Kukawa giza adhimu,
Ikashuka mvua mbinguni, Maji mekundu ya damu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wakati walipomchinja, Adui walifurahi,
Mwili na waliuacha, Ili aponde ngamia,
Na mtoto wakamchinja, Bila ya kumhurumia,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wanawake wakachojoa, Shungi zao za kichwani,
Huku wakiwasumbua, Wakatembezwa uraiani,
Kwa ukatili wa kuuwa, Ataulipiza Manani,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Kile kichwa ikabidi, Kama si kichwa cha mtu,
Kikapelekewa Yazidi, Akikanyage kwa Fimbo,
Fikra za mkaidi, Si kama fikra za utu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Yazidi aliona vema, Hajui ameangamia,
Ndani ya Jahanama, Ndiko alikoingia,
Na maji yaja hima, Ndiyo anaumiya,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Hapa ninahitimu, Shairi nimekomesha,
Ingawaje nina hamu, Yakutaka kuzidisha,
Rabbi unirehemu, Kwa haya yangu maisha,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Na kila msikiaji, Mwenye roho ya mahaba,
Rabi mwondolee balaji, Mpokelee kila toba,
Yarabi utufariji, Kwa baraka ya Habiba,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Muienuddin Chishti Ajmeri Asema:

Shah ast Husain Badshah ast Husain
Din ast Husain Din Panah ast Husain
Sar daad, Na daad dast dar daste Yazid
Haqqa ke Binae Lailah ast Husain.

Maana yake:

Husain ni Mfalme (ni Bwana)
Husain ni Mfalme wa Wafalme (ni Bwana wa Mabwana)
Husain ni Dini, Husain ndiye mhifadhi wa Dini
kichwa alikitoa, bali hakutoa mkono wake kwaYazid
Hakika Husain ndiye msingi wa Lailaha illallah.

Yaa Husain, yaa Husain kullu yawmin Aashura
Kullu ardhin Karbalaa, yaa abal ahraar x 2

Yaa Salilul ambiyaa, anta Imamul atqiyaa
Yaa abal ahraar x 2

Yaa Kahfil mustajirrin, yaa shariul mudhnibiin
Yaa abal ahraar x 2

Yaa ilma fikulli waad, yaa imama filjihadi
Yaa abal ahraar x 2

Laa ilaha illa llah, yawmi twaffi–laa nansaa x 2
Yaa abal ahraar x 2

Yaa sar khata thairin, Haihata annastakini x 2
Yaa abal ahraar x 2

Ya kahfa wal mu'utamad, amta zaadi wa sanaad x 2
Yaa abal ahraar x 2

Silmun liman saalamakum, Harbun liman haarabakum x 2
Yaa abal ahraar x 2

Aaala rabbul kainati, fajrana hatma liat x 2
Yaa abal ahraar x 2

Yaa min haja filhayat, yaa qudwata bil abat x 2
Yaa abal ahraar x 2

Yaa man jismuhu saliib, yaaman shaibuhu khatib x 2
Yaa abal ahraar x 2

Yaa madhlumu yaa dhaman, abkaital insi wal jani x 2
Yaa abal ahraar x 2

Yaa man tabkiikas-samaa, yaa sayyida shuhadaa x 2
Yaa abal ahraar x 2

Yaa safinatun-najaat, anta muhyii fil mamat x 2
Yaa abal ahraar x 2

Yaa imamal muttaqin, farrat bil haqqil mubin x 2
Yaa abal ahraar x 2

Nahjuka nahjurrasuul, saatwiu yahdil anam x 2
Yaa abal ahraar x 2

Amta baaki lantazul, Haadiu Nahju rrasuli x 2
Yaa abal ahraar x 2

Allahu akbar Allah, yaa Husain ya Husain
Allahu Akbar Allah yaa Husain ya Husain

Aliyyu yandubu wayaqulu yaa Husain ya Husain x 2

Al-Hasani yandubu wayaqulu yaa Husain ya Husain x 2

Rasulu yandubu wayaqulu yaa Husain ya Husain x 2

Azzahra tandubu wataqulu yaa Husain ya Husain x 2

Fatima tandubu wataqulu yaa Husain ya Husain x 2

Sakina tandubu wataqulu yaa Husain ya Husain x 2

Jibrilu yandubu wayaqulu yaa Husain yaa Husain x 2

Al-ardhu yandubu wayaqulu yaa Husain yaa Husain x 2

Assamaa tandubu wataqulu yaa Husain yaa Husain x 2

Yaa Abbas yaa Abbas
Ya madhulum fii Karbalaa x 2

Yaa Madhulumaa fii Karbalaa
Yaa man mata wahuwa atshan
Ya madhulum fii Karbalaa x 2

Bakati Sakina ladaa Karbalaa
Wa Muhammadahu banatuka sabaya
Yaa madhulum fii Karbalaa x 2

Bakati ssamaa'u liqatilil Husain
Wa sibtwahu ladaa Karbalaa
Yaa madhulum fii Karbala x 2

Yaa madhulum fii Karbalaa
Wa nazifaahu fii Karbalaa
Yaa madhulum fii Karbalaa x 2

Ra'asuhu Husain fawqaa rrimahi
Sibtun-nabiyyi muqattalaa
Yaa madhulum fii Karbalaa x 2

Sibtur-Rasuli muqqattalaa
Waa sibtwahu fii Karbalaa
Yaa madhulum fii Karbalaa x 2

Waa Husainan waa Husainan waa Husainaa x 2

Waa Husainan swaha Jibriilu hazinaa
Ya srakhul kawnu bukaa'an wa aninaa

Qad Qadha ssibtu ghariban fii tufuuf
Wahdahu haafat bihi tilka sufuuf
Min rimahin au nibalin au siyuuf
Thumma dhulman Qatwau minhul watiina

Waidha bii ssibtwi fii twaffi gharib

Jismuhu saa haati fii harbi saliib
Ma’ahu rahtul ubati swabirinaa

Masaqawhul–maa'fii Yawmil–fajii'li
Huwa dham aanin yunadi sama uuh
Maata atshanan walam yusqal mainaa

Innahum Lam yarhamu hataa rradhii
Wa Husainu ssibtwi kassaddil–manii
Nah'wu qawmil ghadri maa maddal yamiinaa

Maata alul wahyi walkhatbijaliil
Ma baqaa minhum siwaa shakhu su aliil
Wanhisaauu thakila tuu fil–awiil
Qad faqadnal ahla dhulman mal baninaa

Yaa Lailatal–ashri tuul
Qad zaada fiiki nnuhuul
Wadidtu min Qibali kuumi
Yaa hunu waq rrahiil

Bikarbalaa mudh–nazalnaa
Alimtu inda nnuzuul
Biannana sawfa nabqaa
Bila hami wwakafiil

Wadhaaka aadhamu thatwabi
Min zamani jaliil
Yumsil Husain Qatiilaa
Wa Yaalahu mun katiil

Fayaa dumuiya siilii
Alayhi kulla masiil
Thumma nthanat bintu twaha
Bi–Ibrati wa awiil

Tukhatibu–llayla laakim
Khitwabuha an dhuhuul
Taqulu la tubdi subhaa
Wadha minal mustahiil

Tunasikitika sana kwa kifo chako Husain
Ewe Husain ya shahida Karbala x 2

Mal–uni alofika kukuua ya Husain
Na Mungu atayaweka makazi yake motoni
Ewe Husain ya shahida Karbala x 2

Mbingu zilitikisika kwa kifo chako Husain
Majabali kupasuka kwa khofu na kwa huzuni
Ewe Husaini ya shahida Karbala x 2

Upanga uliushika ili kutetea dini
Kuchezewa yetu dini Husain hukuridhika
Ewe Husain ya shahida Karbala x 2

Tarehe za tuonyesha kwa kifo chako Husain
Husain umeondoka umeacha pengo kubwa
Ewe Husaini ya shahida Karbala x 2

Tunamuomba Manani amiani mal–uni
Amlani hayawani Yazidi na jeshi lake
Ewe Husain ya shahida Karbala x 2

Kiitikio

Mzuri sana Husaina, Wallahi na kuapia
Giza ilituenea,hapo ulipouliwa

Ee mwema mwana amani, umekufa kishahidi
Kunusuru hasa dini, ya wetu Mola wadudi

Umejitolea muhanga, ewe mwana wa Hashima
Ili kuhifadhi mwanga, Nuru kubwa ya Karima

Kila lote la azizi, kwa Rabuna umetoa
Bila kujali ajizi, hadi kufa kuokoa

Wanao wenye tohara, Nduguzo waso kifani
Masahaba we imara, umetoa uwanjani

Kunusuru haki kweli, mfano wako kuiga
Ujabali wenye dhili, kupambana bila woga

Kuishi na madhalimu, kamwe neema hapana
Ni kudhili jahanamu, maisha hayana maana

Husain akafahamu, Ikawa hakuna budi
Mauti yake metimu, Dhiki imeshawazidi
Na kweli yake damu, Wazee kwa auladi
Adui watachezea, Roho zikiteketea

Adui pasi kuchoka, Kiu ilo kubwa mno
Waka mwandama mpaka, Joto lisilo kifano
Karbala wakafika, Vijana wazi midomo
Kusudi la mwandama ,Maji wanahitajia

Furati wakaushika, maji wanywayo wanyama
Pasi nafasi kutoka punda, farasi na kima
Mto wakauzunguka, Mjukuu wa Hashima
Na maji wakijinywea, Adui wakazuja

Kiu ikazidi sana, Dhiki ilipo wazidi
Na joto likawabana, Akamuona waladi
Imamu na wakewana, Asifanye ukaidi
Dhiki ikiwazidia, Adui akawendea

Kile kijana swaghiri, Kijana kikalalama
Imam wetu Amiri, Chembe kimeshika nyama
Tamaa hakuikata, Na damu mwili mzima
Ya maji kumpatia Mikononi akafia

Adui wasikubali, Mikononi mwa Imamu
Japo lau tone mbili, Yote ikajaa damu
Muhali wakaratili, Na roho yake ghulamu
Pasi Imani kuingia Ikaiaga dunia

Alipo akikariri ,Ukazidi ukaidi
Imamu akihubiri, Na jeshi la mafisadi
Alipewa takiswiri, Ikawa hapana budi
Chembe wakamrushia Roho zikiangamia

Waliondoka huruma, Basi huu ndio mwanzo
Wakawa kama wanyama, Wakazidisha mkazo

Pasi kujali dhuluma, Pasiwe hata pumbazo
Roho zikiteketea Vitoto vikiumia

Imam Husain (*a.s.*) *Asema:*

Imam Husain (a.s.) alipokuwa safarini
kwenda Karbala alisema:

"Kama Dini ya (Mtume) Muhammad (s.a.w.w.)
haiwezi kuendelea ila
kwa kukitoa mhanga kichwa changu,
basi upangana uje ukichukue".

Kwa jina lako Jalali nasema yenye ukweli
Ya Husaini Bin Ali niwe nikihadithia

Mama yake ni Fatima, na babu yake Hashima
Na Madina mji mwema, ndiko alikozaliwa

Na Sayidina Husain, kaka yake ni Hasan
Akiwapenda amini, kisha akiwa sifia

Mtume amebaini, ya kama huyu Husaini
Na mwingine ni Hasani, Peponi wataingia

Yaani wao ni mabwana, wa peponi vijana
Subhana maulana, wote amewaridhia

Ni mwezi wa Shaabani, alozaliwa Husain
Na siku yake yakini, ni jumanne sikia

Mwaka wa nne Hijira, ndio kazawa mbora
Na siku ya saba mara, kamwakikiya Nabia

Mtume kamwadhinia, sikioni la kulia
Kinywa kamsugulia, kwa mate halafu nia

Alikuwa ni mzuri, wa umbo la kunawiri
Sura kama ya bashiri, kwani kamshabihia

Akipigania dini, kwa udhati moyoni
Hajali nini na nini, ila dini ya jalia

Husaini akiwa Maka, aliupata waraka
Kuwa aende haraka, Iraqi kum–baiya

Watu wangu simameni, twende Iraqi mjini
Aliwambia Husaini, nao wakafuatia

Husaini aliambiwa, huko acha kuendea
Twakusihi kusikia, huko hapatakufaa

Abdallah wa Abasi, Kasema kinga nafsi
Zao japo wafuasi, japo na watoto pia

Wende wewe peke yako, sio na ahali zako
Bwana kwa hisani yako, shika ninayokwambia

Bwana Husaini kasema, Kwenda huko ni lazima
Litalonipata ni jema, Mimi nimesafi nia

Nikenda wakiniuwa, peponi nitaingia
Kwani nimesafi nia, dini kuisimamia

Liwalo lote na liwe, Iraqi ni paendewe
Sio mimi nihofie niache kupaendea

Hapo Seyyidi Husaini, Katoka Makka mjini
Na watu wake sabini, Wote wakamfatia

Wenye farasi yakini, walikuwa thalathini
Wengine arubaini, kwa miguu ilikuwa

Alipokuwa njiani, wakazidi yakini
Mia moja khamsini, ndio waliozidiya

Hao mia khamsini, walirudia njiani
Hawakumfata Husain, hadi Iraqi sikiya

Husaini na watu wake, ni Iraqi Wapafike
Na taabu iwafike, kwa humo Karbala

Mto ulio karibu, nae Husaini Muhubi
Alizuiwa ajabu, na maadui kutumia

Maji wakazuiliwa, wasiwe wayatumia
Kambi akajipigia, bwana Husaini sikia

Akawa maji anyimwa, huku kiu chawauma
Watoto wanalalama, kwa vile wanaumia

Husaini na watu wake, ati wao wateseka
Na maji yasitumike, kunywewa na watu hawa

Hapo Husaini hakika, vikali aliteseka
Watoto walalamika, Baba! Baba! twaumia

Jeshi hilo lilikuwa, kabisa lamzuia
Husseini kukaribia, maji yale kutumia

Watoto waliumia, kwa kiu kuwazidia
Kati yao alikuwa, mtoto mdogo pia

Mtoto huyu ni Ali, alizidiwa kikweli
Zeinabu binti Ali, sana sana alilia

Machozi yalimtoka, mengi yakatiririka
Akayafonza hakika, mtoto kujimezeya

Zeinabu binti Ali, ni shangazi lake Ali
Kwa ala kulihali, machozi maji yakawa
Hata ile siku ya Ashura, kwa mwezi kumi dhahira
Muharamu ndio mara, wakaanza kuuwawa

Kwanza wafuasi wake, kisha wa nyumbani kwake
Alibaki ye na chake, kijitoto kikilia

Umri miezi sita, hivyo hanavyo matata
Hivyo maji angepata, yangali msaidia

Mtoto mchanga yule, wakampiga mishale
Na mtoto pale pale, aliiaga dunia

Kisha wakamzunguka, Husaini mwenye baraka
Wakamuuwa hakika, nae kaaga dunia

Baada ya kumuuwa, hema moto walitia
Hata wakawachukua, banati zake Nabiya

Wakawafanya mateka, kisha wakawapeleka
Huko Kufa kupafika, bila kuwahurumia

Ni kwa Ibni Ziyadi, ndiko iliko wabidi
Gavana wake Yazidi, yeye ndie alikiuwa

Hivyo watu wa Iraqi, walikataa haki
Kumuuwa mwenye haki, kipenzi chake Nabia

Kuuwawa kwa Husaini, Ni jambo lenye huzuni
Katu haiwezekani, machozi kuyazuia

Machozi shuti kutoka, na watu kuhuzunika
Kwa kipenzi msifika, kinyume alofanyiwa

Ewe Seyyidi Husaini, ulotoka duniani
Kwa kupigania dini, peponi wenda ingia

Umekufa ni shahidi, hivyo ni kama zawadi
Allahu Mola wadudi, shahidi kakwandikia

Waswalatu wa Salamu, zimfikie Hashimu
Na Husaini Muadhamu, na walio bakiya

Na: Saidi Musa
Zanzibar

Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi Asema:

Imam Hasan na Imam Husain (a.s.) wameuhurisha
Uislamu kutokana na utumwa wa Wafalme na hivyo basi,
Wameuhifadhi kutokana na uharibifu daima.

Wafalme watakuja, na Wafalme watakwenda,
lakini Uislamu utadumu milele.
Kwa Uislamu, majina matakatifu
ya Hasan na Husain yataangaza milele.

Vikali mmeteswa na pepo mtaingia
Na waliowatesa motoni wataingia

Aliy Bunal Husaini kauwawa Karbala
Mishale pia vyuma vyote kuwa juuye

Aliomba ruhusa kwenda kupigania

Akapigwa mshale na Ibn Fadhili
Kichwani mwake huyo Aliy Ibunil Husaini

Ashahidul Abasi kauwawa vibaya
Mikono ilikatwa yote miwili pia

Imam wetu Husain kauwawa Karbala
Mikuki na mishale vyote kuwa juuye

Kadhulumiwa Husaini huo mji Karbala
Humo usoni mwake mawe alirushiwa

Vitoto vililalama midomo ilikauka
Maji wahitajia adui wamezuiwia

Midomo ilipasuka damu pia zilitoka
Akina mama pia maziwa hayakutoka

Imamu wetu Husaini alichinjwa kinyama
Na hao maluuni fii ardhi Karbala

Ya Aliy ya Aliy ya Abal–Husaina
Qutilal–Husaina fii ardhi Karbala
Fii ardhi Karbala Qutilal–Husaina

Kwa Jina la Rahmani
Na Muhammad Amini
Naanza kwa madhumuni
Kwa machungu na kuliya

Siku hizi za Ashura
Twazitaja kila mara
Kwa kubwa mno hasara
Maadui walotiya

Kiswache cha tuumiza
Na roho kutuunguza
Hatuwezi kunyamaza
Mashingo kuvumiliya

Twadhihirisha majonzi

Kwa Imamu na kipenzi
Na nyoyo zina simanzi
Kwa haya yalotokea

Twakumbuka siku hizi
Za vilio na huzuni
Ya kuuwawa Husaini
Mjukuu wa Nabiya

Wallahi tunakatika
Machozi ya miminika
Mitilizi inashuka
Hatuna budi kuliya

Husaini kudhulumiwa
Kwa machungu kuuliwa
Kanyimwa maji kupewa
Yeye na wake dhuriya

Hata watoto wachanga
Wasisite kuwanyonga
Kwa mishale kuwadunga
Na maji kuwazuwiya

Wakamchinja Husaini
Bila kite na imani
Mjukuu wa Amini
Pasina kuzingatiya

Na kisha kichwa kukitundika
Kwa shangwe wakizunguka
Kwa mizozo na dhihaka
Kwa kipenzi cha Nabiya

Tuliye kiliyo gani
Tudhihirishe Imani
Kwa kiongozi wa dini
Huyu walo tuuliya

Walomuuwa Imamu
Wakashika yake damu
Hao ndio madhalimu

Tarikhi inatwambiya

Bila shaka yu peponi
Yeye na tumwa Amini
Ole nao makhaini
Husaini kutuuliya

Kula alo muumini
Atajawa na huzuni
Kwa kifo chake Husaini
Kipenzi cha Hashimiya

Na mengi tukiyaeleza
Maovu ya kuchukiza
Ya akili kushangaza
Na moyo kutosheya

Tumefika kikomoni
Tushukuru Manani
Atupe nyingi Imani
Ya dini kusimamiya

Muliyoko Hadhirani
Amina itikieni
Rabi atiye auni
Dini kuipiganiya

Umetungwa na:

Sheikh Ahmed Sheikh Nabhany
P.O. Box 86876
Mombasa, Kenya.

Hakika ni ujahili
Uovu na ukatili
Kuuwa pasi kujali
Bila ya kuzingatia

Asikiyae Hakika
Moyo utasikitika
Ma machozi yatatoka

Bila yakufikiria

Kwa huyu mtoto wake
Husain kina chake
Muda kiu imshike
Maji akihitajia

Kufika kwa makafiri
Husain alopojiri
Na mwana huyu saghiri
Maji alimuombea

Maadui wasijibu
Kwa kuwazidi ghadhabu
Mmoja wao kajibu
Mshale kuutumia

Jibu lake ni mshale
Kumchoma mwana yule
Akafia pale pale
Kifo cha kukusudia

Hapo ndipo Husain
Kwa uchungu wamoyoni
Akaingia vitani
Bila tena kungojea

Husain akapigana
Kishujaa kukazana
Akauwa wengi sana
Kwa nguvu zake Jalia

Naye mwisho kifo chake
Afanyeje peke yake
Akafa hali yu pweke
Shahidi akajifia

Husain amefariki
Hali yukatika haki
Na hao ni yao dhiki
Walomtenda ubaya

Naanziliza kauli
Kwa jina lake Jalali
Na Swalawati Rasuli
Na–ali zake pamoja

Mswiba ulo adhimu
Kwa mwezi wa Muharramu
Dhuriya zake Hashimu
Karbala wakingiya

Hadithi imetuwambiya
Rasuli ameuswiya
Wapendwa wake dhuriya
Kinyume wakatumiya

Umati walibadili
Mahabba yao kwa Ali
Ikawa ni kuwadhili
Na maji kuwaziwiya

Yasitoshe walofanya
Ya Mtume kuyakanya
Dhuluma wakamuonya
Vijana kumuuliya

Hawakujali hishima
Ya Sayyidati Fatima
Vijana waliye wema
Wa Haidari Aliya

Sina budi nitalia
Kukosa kuwatetea
Iwe kwetu mazoweya
Ashura ikingiliya

Hadithi walisahau
Mapenzi wakadharau
Wakawauwa na kiu
Furati wakangaliya

Walikunywa Kauthari
Maji mema ya fakhari

Pamoja na Answari
Dini waloitetea

Yalopita tayakidhi
Kwa Tumwa nipate radhi
Na kwa Mungu ni fawidhi
Na Aya kiisomeya

Inna Lillahi Wa Inna Ilaihi Rajeun

Sharif Mohammed Ahmed Al–Husaini
Jomvu Station, Mombasa

Naanziliza kwa jina
Lake yeye Subhana
Mola asiye kijana
Wala mke asiliye

Ndie watangu natangu
Kabula ya ulimwengu
Muumba nchi na mbingu
Milele Atabakiya

Asie na mshirika
Na wala hakuzalika
Ameketi pasi shaka
Enzie imetimiya

Sasa penda kuweleza
Kisa chenye kuchukiza
Na moyo nitaukaza
Hadi mwisho kufikiya

Ni rafiki wa Rasuli
Muhammadi mur sali
Husaini mwana wa Ali
Na Fatima Hashimiya

Kipenzi chake Nabiya
Kuliko viumbe piya
Uhai wake sikia

Husaini akimwambiya

Wewe mtu wa peponi
Huna shaka asilani
Apendae kubaini
Namtizame Husaini

Baada kufa Rasuli
Muda ulipotawili
Na Alii mjamali
Alipoaga duniya

Kukazidi wasiwasi
Ulimwengu ukahisi
Pasiwe mwenye nafasi
Matumbo kupiganiya

Baada yote kufika
Na damu zikimwaika
Waso haya wakatoka
Vita wakaandaliya

Vikaandaliwa vita
Na mengi mno matata
Umbea nausalata
Vigaro vikatimiya

Vigaro vya mahasidi
Nyoyo zenye ufisadi
Chini ya yeye Yazidi
Vitani wakaingia

Husaini yuko ndiani
Kutaka ihami dini
Kuwapinga mashetani
Nakuituza duniya

Kwa moyo uso imani
Majeshi yakawa kani
Na damu waitamani
Ya Husaini na dhuriya

Wakawa wajikatakata
Watakayo washapata
Na Imamu washamwita
Mjini kwao kwingiya

Habari hiyo hanayo
Amekaza wake moyo
Kumbe mambo sasa siyo
Mauti yamngojea

Yunjiani enda zake
Akaweta watu wake
Waume na wanawake
Na radhi akawiliya

Kuwajuza kwa yakini
Hila zote kwa makini
Pasipo matumaini
Iraqi kufikiliya

Kawambiya kimbieni
Atakae samahani
Ila mimi niwacheni
Nimuhali kukimbiya

Baada yeye kukuli
Wengi hawakuhimili
Kama vile mafahali
Nyumbani wakarudia

Akabakiya Husaini
Na dhuriya wa nyumbani
Na baadhi ikhiwani
Akali wakasaliya

Alipofika Iraqi
Jamii ya halaiki
Furaha na kujinaki
Jeshi likamwingilia

Akawa hana namna
Pande zote amebanwa

Pamwe na wake vijana
Wapi watakimbiliya

Akasema kwa lafudhi
Kwa fasaha na mahadhi
Adui kuwapa radhi
Kuwatajia Jalia

Akawaonya mifano
Hati zao za mkono
Barua zilizo nono
Walizo kumwandikia

Kayesha yote maneno
Wala pasipo usono
Yote yasiwe ni neno
Yao wakashikilia

Wakamuonya adhabu
Na nyingi mno sulubu
Zimewaingia ghadhabu
Bila sababu ya njia

Adui pasi kuchoka
Wakamwandama M-maka
Karbala wakafika
Kusudi wa mwandamiya

Furati wakaushika
Pasi nafasi kutoka
Mto wakauzunguka
Na maji wakijinyweya

Kiu ikazidi sana
Na joto likawabana
Imamu na wake wana
Dhiki ikawadhidiya

Ikawa hakuna budi
Dhiki imeshawazidi
Wazee kwa auladi
Roho zikiteketea

Kiu ilo kubwa mno
Joto lisilo kifani
Vijana wazi midomo
Maji wanahitajiya

Maji wanywayo wanyama
Punda farasi na kima
Mjukuu wa Hashima
Adui akazuwiya

Akenda kwao salama
Karibu roho kutema
Abdallah anawana
Kwa kiu kumzidiya

Kile kijana swaghiri
Imamu wetu Amiri
Tamaa hakukasiri
Ya mali kumpatiya

Adui wasikubali
Japo lau tone mbili
Mahali wakaratili
Pasi imani kuingiya

Ndipo akikariri
Imamu akihubiri
Alipata takisiri
Chembe wakamrushiya

Wakamba ha ndiyo maji
Katu huyaonji maji
Mnyweshe yamfereji
Ni leo mtatubiya

Kijana kikalalama
Chembe limeshika nyama
Na damu mwili nzima
Mikononi kikafiya

Mikononi mwa Imamu
Yote ikajaa damu

Na roho yake ghulamu
Ikaiaga duniya

Katu wakamba adui
Maji yetu situmai
Mtayaona jamii
Kinywani hamtotiya

Ukazidi ukaidi
Kwa jeshi la mafisadi
Ikawa hapana budi
Roho zikiteketeya

Basi huu ndiyo mwanzo
Wakazidisha mikazo
Pasiwe hata pumbazo
Vitoto vikiumiya

Kajaribu kwa upole
Kuwaeleza walo pale
Maji yote yako tele
Japo tone kutumiya

Akenda huko karibu
Kiu ilimughilibu
Alipotaka jaribu
Chembe kikamuingiya

Kikamwingia Imamu
Chembe chao mahasimu
Mdomoni kikadumu
Na damu ikamweneya

Huku kiu imemshika
Damu ikichirizika
Msiba umemfika
Hana pakukimbiliya

Kakishika kakizuwa
Kwa nguvu akakitowa
Kamshukuru Molawa
Muumba wa waja piya

Zikazidishwa sulubu
Mno na nyingi taabu
Rafikize wakaghibu
Mauti kuyandamiya

Rafiki wakaanguka
Imamu kumzunguka
Na damu zikimwaika
Akawa aogeleya

Katikati kwenye damu
Adui wakakalimu
Katu yako hayatimu
Mauti yakungojeya

Mauti yenye taabu
Usumbufu na adhabu
Yatakufika karibu
Kaa ukiliadhaniya

Ni leo, leo ni leo
Utaiona kwa leo
Na wote hao watu
Wote tutawalemeya

Kakalimu muungwana
Kamshukuru Rabana
Na Molawe kalingana
Na dua kujiombeya

Akatamka Husaini
Kamwambia Mola manani
Kwako wewe shukrani
Nyoyo zimefurahiya

Hatuna katu huzuni
Kwa ulio yasaini
Mauti twayatamani
Kuliko kuangukiya

Vita vikauma sana
Pasipo kusemeyana

Na Imamu akawana
Pasi nyuma kurejeya

Lakini ifae nini
Kwa adui elfeni
Na ziyada ilondani
Husaini akalegeya

Akalegeya kwa dhiki
Aloikuta hilaki
Asimpate rafiki
Huruma kumuoneya

Ukweli ulodhihiri
Ikakabili ni shari
Haikuweko ni siri
Shida zikawachachiya

Kutamka kwa upole
Pasipo nyingi kelele
Sahibuze kuwambile
Atakaye kukiribiya

Usiku huo gizani
Kawambia kimbiyeni
Na mimi radhi moyoni
Na dua nawaombeya

Jamii wakakataa
Heri kwao kujifia
Kuliko kuyakimbia
Mauti wakaridhiya

Adui likadhihiri
Moyo umetahayari
Na upesi ikaswiri
Imamu kumjiliya

Mtoto wake Husaini
Naye alipobaini
Karuka pasi makini
Amie kumteteya

Pasi khofu wala shaka
Adui akamshika
Na maneno katamka
Msihaya kamwambiya

Kamwambiya huna haya
Bure wayatenda haya
Utaikuta hizaya
Mbele ya Mola jaliya

Adui likazunguka
Mtoto akamshika
Husaini akimtaka
Kijana kumuusiya

Huku mepiga pambaja
Na adui huko waja
Na huku akiwapiga
Mpaka mwisho kufikiya

Yakamzidi machungu
Akamsabihi Mungu
Akaaga Ulimwengu
Mjukuu wa Nabiya

Ghafula akijiliwa
Roho yake ikatwawa
Adui lake Moliwa
Imamu akamwendeya

Akamwendeya kwa dhati
Akamendesha mauti
Jiadui afiriti
Dharuba kumwemezeya

Alipokufa Husaini
Yalitimu thelathini
Na tatu yaliyo ndani
Mafumu yalowingiya

Kuna tena thelathini
Na nne mwake mwilini

Panga za hao wahuni
Mwilini zimesaliya

Mbali mengi majaraha
Kuyataja ni karaha
Moyo hauna furaha
Kwa Imamu kujifiya

Ndio huo mwisho wake
Hiki ndicho kisa chake
Cha Imamu tusichoke
Milele kujisomeya

Walipokwisha saini
Adui wakabaini
Sasa hii ni yakini
Ushindi umewajiya

Wakendewa majohari
Mabanati wa Amiri
Matekani wakaswiri
Huku wakiwachezeya

Pasi haya za uso
Wakaona ni kifani
Kuwatia taabani
Jamaa zake Nabiya

Wakazidisha jeuri
Wala pasipo na siri
Na kichwa chake Amiri
Fumoni wakakitiya

Huku wakikichezeya
Na huku wakiimbiya
Pasi imani kuwaingia
Wote wamefurahiya

Njiani walikipita
Nyoyo zao mezipata
Zimekwisha jaa vita
Shetwani amewaingiya

Alipopata habari
Kwa ambayo yamejiri
Yazidi akaamuri
Ili kwehwa kumwiliya

Furahani vibaraka
Haraka kukipeleka
Kwa Yazidi kikafika
Meyowe kufurahiya

Akawa akichezeya
Na vijiti kukitiya
Huku akimbiliya
Chini kukiumbiriya

Aso haya wala dini
Yazidi akatamani
Uchunguwe wa moyoni
Utatowa kwa duniya

Na huku akikigota
Meno akiyaambata
Uovu na usalata
Hakuna alodhaniya

Ajabu hii ajabu
Kwa kijanache swahibu
Kumfikiya ikabu
Wala pasipo hatiya

Muili ukiwa mbali
Kijana cha Murisali
Wakawachiwa mahuli
Na nyama kukitezeya

Basi haya ni mauti
Walotenda asherati
Lakini kwao laiti
Milele wamejutiya

Walitenda pasi haya
Dini kutotegemeya

Ya Mola kuyachezeya
Pasi nyuma kurejeya

Yapasa tuyalilie
Mauti yake Husaini
Islamu natulie
Kwa kifo chake Husaini

Hapa napenda kukoma
Hadithie kuisoma
Bali mengi sikusema
Dhiki nikiisikiya

Kisomoni waungwana
Majumbani na vijana
Mpate jua maana
Mambo yaliyotukiya

Yatupasa Isilamu
Machozi hadi ya damu
Kumliliya Imamu
Kwetu imetupasiya

Rabi atamtukuza
Peponi kum-bakiza
Kuzidi akimjaza
Neema kumshushiya

Hapa naweka kalamu
Nimefikiya makamu
Wala mbele siyo tamu
Hapa nitakomeleya

Na: Masoud Abdallali Muh'd,
Mombasa - Kenya

Imam Shafii Asema:

Husain! aliuliwa shahidi pasi na makosa yoyote
na kanzu yake ikatapakazwa wekundu.

Ikiwa dhambi zangu ni kuwapenda
Watoto wa Mtume Mohammad (s.a.w.w)
basi ni dhambi ambazo sitatubia.

Kwa sababu ya Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w)
Ulimwengu mzima ulitetema
na majabali na milima ilikaribia kuyeyuka.

Ni nani atakayemfikishia Husain ujumbe wangu na hata kama nyoyo zatukia?

Nawapa na taarifa
Japo kuwa walikufa
Walikuwa wana sifa
Njema zilotimilia

Walikuwa watukufu
Tena ni waaminifu
Walo na njema sharafu
Alowajazi Jalia

Walikuwa Maimamu
Kuongoza Isilamu
Mashujaa walotimu
Dini kuipigania

Walikuwa watu wema
Vijana wenye heshima
Akiwapenda Hashima
Wajukuu wa Nabiya

Walikuwa wenye dini
Maovu hawathamini
Na nyingi mno imani
Nyoyoni ilowangia

Walikuwa na huruma
Isilamu wenye hima
Toka kwa watu wazima
Na vijana wote pia

Walikuwa wasifika

Duniani kutukuka
Tena waliyoumbia
Kwa uzuri na tabia

Walikuwa makarimu
Huwezi kuwalaumu
Kisha ni wenye ilimu
Ya dini na ya dunia

Walikuwa wafalume
Wajukuu wa Mtume
Mashujaa wenye tume
Vitani kushambulia

Sifa zao ni kathiri
Tena zote ni nzuri
Wala hazina akhiri
Wallahi zimezidia

Jambo jengine ni hili
La majonzi ikhiwani
Hiki si kisa cha pili
Ambacho ni cha huzuni
Ni cha kijana rijali
Mtoto wake Husaini

Kadhulumiwa Husaini
Na wake mwana mchanga

Naye kafa madhulumu
Kijana wa mikononi
Muovu huyo Khasimu
Adui aso imani
Bure kaimwaga damu
Ya kijana maskini

Kadhulumiwa Husaini
Na wake mwana mchanga

Kifo chake ni dhuluma

Kijana huyu yakini
Adui aso huruma
Aso Imani moyoni
Kwa mshale kamfuma
Ukamwingia mwilini

Kadhulumiwa Husaini
Na wake mwana mchanga

Mshale ulimdunga
Mtoto wake Husseini
Ikawa hapana kinga
Ya kuiyepuka zani
Akafa mwana mchanga
Kiumbe cha Rahamani

Kadhulumiwa Husaini
Na wake mwana mchanga

Ovu liso wezekana
Kupata chake kifani
Kiumbe chake rabana
Kilo safi cha peponi
Walimu–uwa kijana
Bila kosa asilani

Kadhulumiwa Husaini
Na wake mwana mchanga

Huyo ni wake uwele
Alo mughuri shetani
Alomdunga mshale
Kipenzi chake amini
Naye pia vile vile
Ataingia motoni

Kadhulumiwa Husaini
Na wake mwana mchanga

Kwa kumuuwa kijana
Malaika kwa yakini
Hata akatubu sana

Haipati samahani
Adhabu yake rabana
Kwake haiwezekani

Kadhulumiwa Husaini
Na wake mwana mchanga

Imam Husain (*a.s.*) *Asema:*

"Kufa kwa heshima ni bora kuliko kuishi kwa aibu".

Kukuomba sina budi
Ya Razaku ya Wadudi
Ili utimu mradi
Yote nalo kusudia

Sikutaka kusimama
Mengi mno kuyasema
Ni mambo kunisukuma
Ni lazima kuelezea

Natokeza hadharani
Kwa ufupi nibaini
Yalomfika Husaini
Ya Rabbi niafikia

Yale ni mambo adhimu
Yalomfika Imamu
Sina shaka mwafahamu
Nami tawahadithia

Ule mwaka wa sitini
Wahijira sikieni
Kaondoka duniani
Muawiya kajifiya

Yazidi alitangaza
Nchi zote kaeneza
Dini ataiongoza
Ili watu kum-baiya

Barua aliandika
Madina kaipeleka
Kwa Walid ikafika
Nae akimwelezea

Kwa makini isomeni
Mfahamu yalo ndani
Kahitaji kura zenu
Isilamu wote pia

Nazidi kuyabaini
Yalio mwangu moyoni
Ni kura yake Husaini
Ufike kumwelezea

Husaini kastakimu
Akasema yakatimu
Huyo ni mtu dhwalimu
Kidini hakutimiya

Kama mimi ni haramu
Kukubali ya dhwalimu
Sitaki wake msemu
Mwambiye sitoridhia

Kwanza yeye nakiburi
Ni mlevi hana siri
Kajaa kila fujuri
Nyote mnamtambua

Sitokuwa chini yake
Hapa na pale afike
Taji hilo silo lake
Hata yeye yamwelea

Mtume alibaini
Kwa Hasani na Husaini
Ni Maimamu yakini
Kila mtu kasikia

Alfu kumi na mbili
Barua ziliwasili

Kwa mjukue Rasuli
Iraq zilitokea

Barua zilimtaka
Husaini huko kufika
Ukhalifa kuushika
Dini kuisimamia

Yazidi si mtu mwema
Sisi sote twafahamia
Na haya tunayosema
Wewe twakushtakia

Husaini hakutwawili
Katuma Ibn Akili
Ili kujua ukweli
Wa mambo yalomfikiya

Alipokewa vizuri
Wadogo hata kibari
Walimfanya safiri
Wa Husaini Msifiwa

Kisha mambo ligeuka
Balozi walimwepuka
Mapanga wakayashika
Muslimu kumuwa

Mwezi nane kutimia
Mfungo tatu sikia
Husaini kashika njia
Iraqi kaelekea

Naswaha zilimfika
Twakuomba kutotoka
Iraqi usije fika
Watu wakakukimbia

Husaini aliwambiya
Hayo yote nasikia
Nitakwenda nadhuria
Mtume kani uswiya

Wakiniuwa sijali
Aliniambiya Rasuli
Kua hayo majangili
Dhuluma watatumia

Alipofika njiani
Aliijua yakini
Ni hayuko duniani
Muslim kauwawa

Iraq waligeuka
Unafiki wakashika
Hivi waja kukushika
Husaini aliambiwa

Ule msiba adhimu
Ulomfika Imamu
Yeye na wake kaumu
Na kizaziche pamoja

Hapa ni pahali gani
Niambiyeni jamani
Ni Karbala jangwani
Husaini aliambiwa

Ibn Saad Omari
Na jeshile waliswiri
Maudhi na ujeuri
Imamu wamfanyia

Unyama walifanyiwa
Na kiu iliwauwa
Na maji kuzuiliwa
Hayo yote watendewa

Kauwawa Akbari
Pia hata Asghari
Na hao watu mashari
Mungu yuwashuhudia

Asghari ni kijana
Ni mdogo tena sana

Na kiu ilimbana
Kwa chembe walimuua

Husaini aliuliza
Fikirini mukiwaza
Kosa gani tulifanza
Kutendewa kama haya

Haya mambo ya huzuni
Alotendewa Husaini
Nashindwa kuyabaini
Ukumbuni kuelezea

Yangu haki mumetwaa
Ya ukhalifa sisawa
Na leo mwanisumbua
Nilipi mwafikiria

Au hamkusikia
Usemi wahashimia
Hapo akiwauswia
Kuhusu wake dhuria

Mama yangu ni Batuli
Binti yake Rasuli
Na baba yangu ni Ali
Waswii wake Nabia

Ya Husaini walimwaga
Damu yake bila woga
Walijifanya wajinga
Ufasiki mewashika

Kijukuu cha Rasuli
Ni Husaini bin Ali
Achinjwa kama ghazali
Wallahi twakulilia

Alipewa kila dhuli
Mwanao ewe Batuli
Ateswa na majangili
Wasio dini sikiya

Walisahau ahadi
Ya Mtume Muhammadi
Na wote ni mashahidi
Mtume akiwauswia

Alimchinja Husaini
Bila khofu na huzuni
Na Mungu si Athumani
Nae atamlipia

Ni kifo chenye kutisha
Tena kina babaisha
Wallahi cha huzunisha
Kila kinapo tolewa

Na Mungu si Athmani
Twalipiwa duniani
Wa kesho wenda motoni
Adhabu yawangojea

Hapo ndipo nitafika
Kalamu chini naweka
Kwa huzuni lonishika
Siwezi kuendelea

Mola atupe Imani
Yakumpenda Husaini
Tuwe nae na peponi
Dua zetu zipokea

Kisha Swala na Salamu
Zende hadi kwa Hashimu
Na alize Maimamu
Hasidi angachukia
.....

Source URL: https://www.al-islam.org/node/40643

Links

[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/40643%23comment-form

[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/40643%23comment-form

[3] https://www.al-islam.org/taxonomy/term/3819

[4] https://www.al-islam.org/library/imam-al-husayn-and-karbala

[5] https://www.al-islam.org/library/general-belief-creed

[6] https://www.al-islam.org/tags/muharram

[7] https://www.al-islam.org/feature/introducing-ahlul-bayt